Hasara ya kuwa na samaki walioharibika.

- Inapoteza wateja wako
- Inapoteza soko lako
- Inadidimiza kipato
- Inakuongezea hasara itokanayo na uharibifu baada ya kuvuliwa
- Inapoteza ajira
- Inapunguza uwepo wa lishe kwa mlaji.

Masoko ya nje.

- Ni eneo lenye kupatikana kipato chenye faida kubwa
- Inachangia maendeleo ya Taifa kwa kuchangia pato la nchi na kukuza uchumi
- Inaongeza uwezo wa nchi kudhibiti mazao yake
- Itasaidia kuunda vikundi vya kibiashara.

Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

AFISA MFAWIDHI WA KANDA

NA MSIMAMIZI WA MRADI (TASP II)

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI

NA VIWANGO KANDA YA ZIWA VICTORIA

S.L.P. 1213 MWANZA

SIMU

+255 28 2550864

+255 754/784 437234

Barua Pepe: nfqcl_mz@yahoo.co.uk

Tovuti: www.nfqcl.go.tz

Imetayarishwa na Maabara ya Kitaifa ya Samaki chini ya Mpango wa TASP II kwa ufadhili wa mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (EDF)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI NA VIWANGO

Masoko ya Samaki na Matakwa yake

TRADE AND AGRICULTURE SUPPORT PROGRAMME II (TASP II)

Masoko ya Samaki na Matakwa yake

Utangulizi.

Soko ni eneo ambalo bidhaa (samaki) inabadilishwa kwa thamani ya fedha. Bidhaa inaweza kubadilishwa soko la ndani (kuuzwa kwenye masoko ya ndani) au kuuzwa masoko ya nje ya nchi.

Umuhimu wa masoko.

- Linawezesha wafanyabiashara kukutana na wateja wao kwa urahisi
- Inasaidia kukuza ushindani wa kibiashara
- Inasaidia upatikanaji wa huduma za pamoja
- Inachangia pato la Taifa kwa kupanua uwezo wa serikali kujiendesha
- Inawezesha uhakika wa uwepo wa usalama wa bidhaa
- Inarahisisha upatikanaji wa takwimu na kusaidia mipango endelevu
- Inaweka mazingira mazuri ya kufanya biashara.

Vifaa na mahitaji ya masoko ya samaki.

Kwa vile bidhaa ya samaki wabichi inaharibika haraka (perishable good), soko linatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Mpangilio wa soko uwe na mfumo wa maji safi na taka
- Sehemu ya kuuzia samaki iwe na kivuli
- Samaki auzwe juu ya meza inayosafishika kirahisi
- Samaki wahifadhiwe katika hali ya ubaridi
- Kuwe na sehemu ya maliwato
- Mhudumiaji wa samaki lazima awe na sare safi
- Vifaa vyote vinavyotumika kuhudumia samaki viwe safi.

Faida za samaki bora.

- Inajenga uaminifu na imani kwa wateja wako
- Uhakika wa soko lako
- Kuongeza kipato
- Inadumisha ajira
- Inapunguza hasara itokanayo na uharibifu
- Lishe bora kwa mlaji